**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**

SHULE YA SEKONDARI MWATISI,
S.L.P 589,
**TUKUYU.**
**SIMU: 0755074268**

**Kumb. Na ..........................** **Tarehe ...............................**

**Jina la Mwanafunzi ............................................**

**..............................................................................**

**S.L.P ...........................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWATISI WILAYA YA BUSOKELO MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.**

## 1.0. UTANGULIZI

Ninafurahia kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujinga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari **Mwatisi Mwaka 2021** shule ya sekondari Mwatisi ipo katika kata ya Kandete Kijiji cha Lugombo.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe **03/01/2021** na Mwisho wa kuripoti ni tarehe **11/01/2021.**

## 2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia.

### 2.1. Sare za Shule.

**a)** Sare ya shule hii ni suruali kwa (Wavulana), Sketi (Wasichana) ya **kijani jeshi 02** na **shati nyeupe 02** na sweta la kijani.

**I. WAVULANA**

- Suruali 2 za rangi ya kijani jeshi zenye mkunjo chini (turn up), zisiwe za kubana.
- Tai ndefu 2 rangi ya kijani jeshi.
- Mashati 2 meupe ya mikono mifupi.
- Viatu jozi 2 vyeusi vyenye visigino vifupi vinavyofungwa kwa Kamba.
- Soksi jozi 2 za rangi nyeupe.

**II. WASICHANA.**

- Sketi 2 rangi ya kijani jeshi ziwe ndefu zilizo chini ya magoti na zikaribie kugusa viatu na ziwe na linda za kawaida (sio linda box).
- Tai ndefu 2 rangi ya kijani jeshi.
- Mashati 2 meupe ya mikono mifupi.
- Viatu jozi 2 rangi nyeusi vyenye visigino vifupi na vinavyofungwa kwa Kamba.
- Soksi nyeupe jozi 2.
- Hijabu nyeupe kwa Waislam

**b)** Rangi ya hijabu ifanane na shati nyeupe.

**c)** Sare ya michezo ya shule hii ni **Track Suit 01 rangi nyekundu** kwa Wavulana na Wasichana.

**2.2.** Daftari za masomo **(09) aina ya Counter book Quire** 4 au **quire 3** au **Quire 2** kalamu,mkebe wa hesabu na Begi (Mkoba wa kuwekea madaftari).
**Madaftari 3 kwa ajili ya Orientation Course** (Madaftari aina ya Msomi).

- **Passport size (Picha 4 zilizopigwa kitambaa cha rangi ya blue bahari).**

**2.3.** Chakula cha kawaida kitatolewa Shuleni ambapo Mzazi/Mlezi atachangia:

a) Mahindi yaliyo kobolewa ndoo ndogo 3 kwa mwaka.
b) Sukari **kilo 3** kwa mwaka.
c) Maharage **BP (5)** kwa mwaka.
d) Pesa kiasi cha **Tsh. 5,000/= (Elfu tano tu)** kwa ajili ya kununua chumvi, na malipo ya mpishi.

**2.4. Mahitaji mengine ya kibinadamu kama.**

**a) Vifaa vya Usafi:**

(i) **Wavulana –** Jembe (Jembe 1 lenye mpini wake na Ufagio mmoja wa Chelewa).
(ii) **Wasichana –** Slesha(Kwanja) moja, ndoo ndogo ya Lita 10 na Ufagio mmoja.

**b) Vifaa vya Chakula cha Mwanafunzi:**

- Kijiko chakula, sahani na kikombe.

### 2.5. Mahitaji ya Kitaaluma:

- Kila Mwanafunzi anapo ripoti aje na **Ream moja** (Ream yenye karatasi mia tano), kwa ajili ya mitihani na majaribio mbalimbali hapa shuleni.

**NB: Kijana wako hatapokelewa shuleni endapo hatatimiza/kukamilisha maagizo yaliyotolewa.**

## 3.0. Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya Mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kimaandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa umakini, kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na:
i) Kutunza mali za umma.

### 3.1. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:

**A.** Wizi
**B.** Uasherati na ushoga
**C.** Ubakaji
**D.** Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika.
**E.** Kupigana au kupiga
**F.** Kudharau bendera ya Taifa
**G.** Kuwa mjamzito/Kupata mimba
**H.** Kuoa/Kuolewa
**I.** Kutoa mimba.
**J.** Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

**K.** Kukataa adhabu kwa makusudi.
**L.** Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0. Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na Mwanafunzi.**

1. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu Hospital ya Serikali fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni.

2. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya wanafunzi Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine.

**5.0. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**“KARIBU SANA”**

**SHULA S.W**
**MKUU WA SHULE.**

MWATISI SEKONDARI,
S.L.P 589,
**TUKUYU.**

**KUMB. NA.**______________________________ TAREHE _____________________.

NAFASI YA KIDATO CHA ___________________________

**AHADI YA KUTII SHERIA , KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE.**

## 1.0. AHADI YA MZAZI/MLEZI.

Mimi ______________________________________________ ni Mzazi/Mlezi wa mtoto ________________________________________ nakubali mwanangu ajiunge na Shule ya Sekondari Mwatisi kidato cha ___________________ Mwaka _____________ Ninaahidi kumpa vifaa/Fedha kama nilivyoagizwa.

Nitafuatilia maendeleo ya Mwanangu kimasomo na /Kitabia na mwenendo kwa kushirikiana na Walimu kwa muda wote atakao kuwepo shuleni Mwatisi pia Nitahakikisha ninamtunza na kumtimizia mahitaji yake ya shule na wakati wa likizo nitamtunza Kitanzania.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ______________________

Tarehe ____________________

**NAMBA ZA SIMU WAZAZI/WALEZI/NDUGU.**

| | **NAMBA YA SIMU** | **UHUSIANO NA MWANAFUNZI** (Mfano: Baba, Mama, Kaka, n.k |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |

## 2.0. AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi _________________________________________nakubali nafasi ya kidato cha ___________ Niliyopewa katika Shule ya Sekondari Mwatisi. Naahidi kuwa nitazitii sheria, Kanuni na maelekezo yote ya Shule. Sitashiriki kwa namna yeyote katika migomo, fujo na makosa ya kijinai nikiwa shuleni au nje ya eneo la Shule. Pia naahidi kuwa nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika sghughuli za masomo, kazi za nje pamoja na michezo kwa muda wote nitakao kuwa mwanafunzi hapa shuleni.

- Dini yangu __________________________________
- Dhehebu langu ______________________________
- Shule niliyosoma _______________________ mwaka ___________ hadi ______

- Sahihi ya ________________________________
- Tarehe __________________________________

**MEDICAL CERTIFICATE FORM**

STUDENT NAME………………………………………………………………………………

To be completed by a Government Medical Officer or a doctor from a recognized health institution in respect of form one entrant. Please examine the above as to her/his physical and mental fitness as a student at this school.

The examination should have to involve the following categories

1. Vision with glasses right …………………………… left……………………
2. Blood pressure ……………………………………………………………………
3. Hemoglobin ………………………………………………………………………
4. F. V. Bleeding ……………………………………………………………………
5. Urine for sugar. …………………………………………………………………
6. Stool for routine examination ………………………………………………
7. Venereal diseases ………………………………………………………………
8. Neurosis ……………………………………………………………………………
9. T. B. Test …………………………………………………………………………
10. Any abnormality
    a) Heart ……………………………………………………………………………
    b) Lung ……………………………………………………………………………
    c) Spleen …………………………………………………………………………
    d) Chest ……………………………………………………………………………
11. Is there any serious disease e.g. Leprosy, Epilepsy, Asthma,

Diabetes ………………………………………………………………………………

Doctor's name………………………………………………………

Signature and official stamp

…………………………………

Date …………………………………